
# Kuwatambua Wanafunzi walio nje ya Skuli na Kusaidia Uhamaji Jumuishi

**Module**

**3**




## Kitabu cha Washiriki


Umetayarishwa kwa ajili ya:

Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

The Norwegian Association of Disabled

Umeandaliwa na:

Enabling Education Network

[Mwanafunzi wa kiume aliyevaa sare za skuli, akiwa amebeba mkoba wa skuli mgongoni anapanda ngazi. Juu ya ngazi pameandikwa ‘Skuli ya Sekondari’. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Watoto hao ni pamoja na mtoto wa kiume aliyevaa shuka aliyoifunga kiunoni akimuangalia mtoto mwengine wa kiume, mtoto mwengine wa kike aliyembeba mtoto mchanga mgongoni akionekana mwenye huzuni, na mtoto mwengine wa kiume aliyevaa miwani myeusi, akiwa ameshika fimbo akiangalia upande mwengine. Chini ya ngazi pameandikwa ‘Skuli ya Msingi’.]

Kazi hii ina hadhi ya kibali cha Creative Commons Attribution Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. Si kwa ajili ya biashara. Kuangalia kivuli cha kibali hicho, tembelea tovuti ya
http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Yaliyomo

Vifupisho....4
Muongozo huu wa nini na ni wa nani?....5
1. Wanafunzi walio nje ya skuli ni nani na kwa nini wako nje ya skuli? ....6
2. Kwa nini wanafunzi wako nje ya skuli Zanzibar? ....19
3. Sera ni nini? ....21
4. Mikakati na suluhisho la kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli ....23
5. Uhamaji katika elimu ni nini? ....25
6. Kipindi cha uhamaji jumuishi huanzia nyumbani....28
7. Mikakati ya kusaidia uhamaji jumuishi....36
8. Jukumu la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu katika kutambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi ....41

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| CBO | Jumuiya za Kijamii |
| EENET | Enabling Education NEtwork |
| NAD | Jumuiya ya watu Waenye Ulemavu Norway |
| NGO | Jumuiya isiokuwa ya Kiserikali |
| OPD | Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu |
| SEND | Mahitaji Maalum ya Kujifunza na au ulemavu |
| SIT | Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli |
| ToT | Mafunzo ya Wakufunzi |

# Muongozo huu wa nini na ni wa nani?

Muongozo huu ni kwa ajili ya washiriki wa jumuiya za watu wenye ulemavu wanaoshiriki katika mafunzo ya moduli ya 3 juu ya elimu mjumuisho.

Moduli hii ina malengo mawili.

1. Kutoa muhutasari kwa jumuiya za watu wenye ulemavu juu ya suala la wanafunzi walio nje ya skuli. Inaangalia vikwazo na masuala yanayohusu kwa nini baadhi ya wanafunzi hawaendi skuli, na mlolongo wa sababu na athari zinazowasababisha kuwa watoro skuli.
2. Kukuza njia ambazo zitatumiwa na skuli ili kuhakikisha wanafunzi walio nje ya skuli, na wanafunzi wengine wote wanapata usaidizi wanaouhitaji kwa ajili ya kipindi cha mpito cha kuingia, kuhama au kuhamia skuli.

Kipindi cha mpito wa elimu huelezea wanafunzi wanaoondoka, wanaofika au wanaojiunga na skuli.

Idadi kubwa ya wanafunzi huwa wanakwenda au wanatoka katika mazingira ya kielimu nje ya muda uliopangwa. Hawa ni pamoja na:

- Wanafunzi walio nje ya skuli ambao hawajawahi kwenda skuli au wameacha skuli.
- Wanafunzi ambao familia zao zinahama.
- Wanafunzi ambao wamelazimishwa kuondoka.
- Wanafunzi ambao hawawezi kwenda skuli kwa sababu ya umbali kutoka skuli, ulemavu ambao hauzingatiwi katika mazingira ya skuli, au umaskini miongoni mwa mambo mengine yanayoathiri jamii zao.
- Wanafunzi ambao wametengwa na skuli zao.

Hakuna njia moja ya kuwajumuisha wanafunzi walio nje ya skuli au kuufanya mpito wa elimu kuwa jumuishi kikamilifu. Hii ni kwa sababu uzoefu wa kila mwanafunzi wa kuwa nje ya skuli, kabla ya skuli au baina ya skuli moja na nyengine, ni tofauti. Kwa hivyo, kila skuli na jamii inayoizunguka inahitaji kubadilika. Kila skuli na jamii inayoizunguka inaweza kuwa na mipango tofauti kwa vikundi tofauti vya wanafunzi na kuanda suluhisho kulingana na muktadha na mazingira yao.

# 1. Wanafunzi walio nje ya skuli ni nani na kwa nini wako nje ya skuli?

Katika mafunzo yaliyopita tuliangalia vikwazo vya elimu mjumuisho. Vikwazo vya elimu mjumuisho ni vikwazo vinavyoathiri **uwepo** wa wanafunzi skuli, **ushiriki** wao katika mchakato wa kujifunza na **ufaulu** wao. Vikwazo hivi vilijumuisha:

- **Vikwazo vya kimazingira**
- **Vikwazo vya rasilimali**
- **Vikwazo vya kimtazmo**
- **Vikwazo vya kisera**
- **Vikwazo vya kiutendaji**

Katika moduli hii ya mafunzo tunaangalia hasa **vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kutokuwepo skuli** - ingawa kiuhalisia vikwazo vingi ni sawa na vikwazo vya ujumuishaji.

## a) Makundi ya vikwazo vya kujifunza

### Mazingira na rasilimali


Mahali ambapo mwanafunzi anaishi kunaweza kuathiri iwapo yuko skuli au la. Kwa mfano, kuna skuli nyingi na ufikiaji rahisi wa skuli katika maeneo ya mijini kuliko vijijini. Katika maeneo ya vijijini, umbali na ukosefu wa barabara nzuri unaweza kufanya iwe vigumu au isiwezekane kwa baadhi ya wanafunzi kufika skuli.





[Maelezo ya picha: Picha inaonesha njia ndefu ya watembea kwa miguu kwenda kati ya vichaka kwenye ardhi yenye vumbi na mawe. Kuna watoto wa kiume wanaochunga mbuzi karibu na njia. Kwa mbali upande wa kushoto kuna skuli. Kwa mbali upande wa kulia kuna kijiji. Watoto wawili waliovalia sare za skuli wanatembea pembeni ya njia ya waendao kwa miguu.]

Katika kipindi cha ukosefu wa maji, wanafunzi, hasa wasichana, wanaweza kuacha skuli kwa sababu wanalazimika kutembea zaidi kutafuta maji kwa ajili ya familia zao.

Rasilimali, zikiwemo za kiuchumi, nyenzo na rasilimali watu zinaweza kuathiri iwapo wanafunzi wako skuli au la. Baadhi ya familia hazina uwezo wa kuwapeleka watoto wao skuli. Familia za kimasikini zinaweza kutegemea kazi za watoto wao ili waweze kuishi. Skuli zilizo katika maeneo yenye umaskini zinaweza kuhangaika kupata vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia na madarasa. Ukosefu wa walimu waliopata mafunzo ni tatizo linaloathiri upatikanaji wa elimu katika skuli.




[Maelezo ya picha. Upande wa kulia nyuma kuna skuli ambayo ina wanafunzi wawili wa kike waliovaa sare wamesimama mbele ya mfanyakazi mmoja au wawili wa skuli na wanafunzi nje ya skuli. Kwa mbele upande wa kushoto kuna watoto wa kike watatu wakiwa hawana sare wamebeba ndoo za maji wanaenda kuteka maji.  wanaangalia upande wa skuli].



[Maelezo ya picha: Darasa lenye msongamano wa wanafunzi wengi wamekaa karibu kwa mistari. Mwalimu anaweza kuonekana kwa mbali mbele akionesha maandishi kwenye ubao. Kuta za darasa na madirisha ziko katika hali mbaya.]

## Mitazamo na imani

Mitazamo ya familia na jamii inaweza kuwa sababu kuu inayowafanya wanafunzi wasiende skuli. Kwa mfano, baadhi ya familia na jamii zinaamini kwamba wanafunzi wenye ulemavu hawapaswi kwenda skuli. Katika jamii nyengine, familia zinaweza kuhisi kwamba watoto wa kike wanapaswa kukaa nyumbani na wasiende skuli. Wazazi na walezi ambao wao wenyewe hawakwenda skuli wanaweza kuona thamani ndogo ya kuwapeleka watoto wao skuli. Mara nyingi ni ukosefu wa maarifa au ufahamu na hofu ambayo husababisha mitazamo hasi.



[Maelezo ya picha: Mwanaume amelala kwenye sofa huku miguu yake ikiwa juu, akizungumza kwenye simu ya mkononi. Ni wazi sio simu ya kazi. Mvulana mdogo aliyevaa mavazi ya shule anashikilia karatasi zenye maandiko akimwelekea mwanaume. Mwanaume anatazama mbali na anainua mkono wake. Uso wake unaonyesha kukasirika.]

## Sera na utendaji

Sera za kitaifa, za ndani na za skuli zinaweza kuchangia tatizo la wanafunzi walio nje ya skuli. Kwa mfano, ikiwa nchi haina sera inayozuia skuli kuwabagua baadhi ya wanafunzi, kwa mfano, watoto wa kike waliopata ujauzito, wanafunzi hao wanaweza kutengwa. Mazoea ya kufundisha na kujifunza huathiri ujifunzaji wa wanafunzi. Wanafunzi wengine huamua kutokwenda skuli kwa sababu hawana furaha. Mazoea ya kufundisha ambayo hayashirikishi wanafunzi kikamilifu na kuthamini michango yao yanaweza kusababisha

wanafunzi kupoteza hamu na kuacha skuli. Wanafunzi pia wanaweza wasiende skuli kwa kuhofia adhabu ya bakora.




[Maelezo ya picha: Kuna mtu amesimama mbele ya darasa akiwa ameshika bakora refu. Anaonekana kukasirika. Anaelekeza bakora kwa mwanafunzi wa kiume aliyesimama mbele yake. Mwanafunzi wa kiume ameinamisha kichwa chake. Kuna wanafunzi wengine darasani wanatazama. Nje ya mlango wa darasa ulio wazi kuna mwanafunzi mwengine wa kiume amesimama kwenye uwanja wa michezo akiwa peke yake kwenye mwanga wa jua bila kivuli.]

## b) Vikwazo vilivyohusiana na namna vinavyoathiri masomo ya wanafunzi

Hakuna sababu moja pekee ya mwanafunzi kuwa nje ya skuli, kwa kawaida kuna mambo mengi tofauti ambayo yanaweza kuchangia tatizo hilo. Kwa mfano, upungufu wa walimu wenye mafunzo unaweza kusababisha skuli kuwa na walimu wachache wasio na ujuzi na madarasa yenye msongomano wa wanafunzi.

Hii inasababisha wanafunzi hao kupata elimu duni. Wanafunzi wanaweza kuwafanya waache skuli kwa sababu hawasomi, na/au wazazi au walezi wao wanaona haina maana kuwapeleka skuli. Skuli pia inaweza kuwa mbali sana na nyumbani kwa mwanafunzi jambo ambalo huathiri mahudhurio yake.

## Vikwazo vilivyohusiana na namna vinavyoathiri masomo ya wanafunzi.



Upungufu wa walimu waliopata mafunzo vizuri



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Wanafunzi wanatoroka skuli na kufanya kazi ya kusafisha na kuuza samaki



Wazazi au walezi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao skuli.




Skuli ipo mbali na makaazi ya wanafunzi

[Maelezo ya picha: Kuna picha sita tofauti zilizounganishwa kwa mishale. Picha ya kwanza inaonesha mchoro wa mwanamke akiwa amekamata bakora na anaonesha maandishi ubaoni. Kuna duara kubwa  jekundu na mstari mwekundu uliopita katikati ya duara la mchoro wa mwanamke huyo. Picha ya kwanza inasema 'Upungufu wa walimu wenye mafunzo sahihi'. Mshale unatuunganisha kwenye picha ya pili inayoonesha darasa lenye msongamano wa wanafunzi wengi wakiwa wamekaa pamoja kwa safu. Mwalimu anaonekana kwa mbali mbele ya darasa akionesha maandishi juu ya ubao. Kuta za darasa na madirisha ziko katika hali mbaya.  Picha ya pili inasema 'Walimu wachache wasio na mafunzo ya kutosheleza na madarasa yenye msongamano mkubwa wa wanafunzi. Mshale unaunganisha kwenye picha ya tatu inayomuonesha mwalimu wa kike akiwa amesimama mbele ya wanafunzi waliokaa kwenye madawati yao. Anaelekeza kidole juu na kuzungumza. Amewapa mgongo wanafunzi wake. Mbele ya darasa mwanafunzi mmoja anachungulia dirishani na mwanafunzi mwengine ameshika kichwa chake kwenye dawati.
Picha ya tatu inasema 'Wanafunzi wanaopata elimu duni'. Mshale unaunganishwa na picha ya nne inayoonyesha mwanamke akinunua Samaki kutoka kwa mtoto wa kiume anaeonekana kunyoosha mkono kuashiria anapokea pesa kutoka kwa mwanamke. Katikati chini yao kuna meza ya Samaki waliopangwa kwa mafungu. Pembeni upande wa kushoto kuna mwnamme aliekaa chini anaonekana anasafisha Samaki, pembeni yake kuna Samaki wengi. Nyuma ya watu hao kuna skuli na kwa mbali wanaonekana wanafunzi wawili, mmoja ni wa kike amebeba mkoba mgongoni anaonekana kuelekea darasana. Na mwanafunzi wa kiume nae pia amabeba mkoba mgongoni anaonekana kuingia katika eneo la skuli. Pembeni kulia kuna bahari.  Mshale unaotokea katika icha yan ne umeelekeza kwenye picha ya tano ambayo mzima mwanamme amekaa mbele ya zuna lililopo juu ya meza ndogo. Mtoto mdogo wa kiume aliyevaa sare za skuli ameshika karatasi zenye maandishi akimuonesha yule mtu aliyekaa. Mtu mzima mwanamme anaangalia upande mwengine mikono yake akielekeza juu. Sura yake inaonesha ni mtu aliyekasirika. Mwisho ambayo inaonesha njia ndefu ilionyooka na isiona hata kivuli. Kwa mbali upande wa kushoto kuna skuli na kwa upande wa kulia kuna kijiji. Watoto wawili waliovaa sare za skuli wanatembea kwa miguu. Picha ya sita inasema 'skuli iko mbali sana na wanakoishi wanafunzi'.]

## c) Vikwazo maalumu vya kielimu kwa wanafunzi

### Umri


Wanafunzi wanapoanza skuli kwa kuchelewa, au kurudia darasa, kuna uwezekano mkubwa wa kuacha skuli kabla ya kumaliza



[Maelezo ya picha: Kuna meza mbili na watoto watatu wa kiume wamekaa katika meza hizo. Upande wa kushoto nyuma kuna watoto wa kike wamekaa na kuelekeana, mmoja aliyekaribu naye akiwa na gongo la kumsaidia kutembelea. Mbele upande wa kulia pia kuna watoto watatu wa kiume. Mtoto wa kiume aliyekaa upande wa kushoto ni mkubwa na anaonekana kuwa na umri mkubwa kuliko watoto wengine katika darasa hilo. Yeye amekaa peke yake na anaonekana hana furaha. Watoto wengine wa kiume wanazungumza na kufanya kazi pamoja.]

### Migogoro na majanga

Migogoro (kama vile vita vya wenyewe kwa wenyewe au mivutano ya kikabila) na majanga (kama vile mafuriko na matetemeko ya ardhi) inaweza kuwa sababu kuu ya wanafunzi kuwa nje ya skuli. Skuli zinaweza kuharibiwa, au familia zinaweza kuhitaji kuhamia maeneo ambayo hakuna skuli. Kwenda na kurudi skuli kunaweza kuwa sio salama au wanafunzi wanaweza kushindwa kabisa kufika skuli .




[Maelezo ya picha: Upande wa kushoto wa picha, kuna skuli yenye paa linalovuja na maji yaliyotuwama katika skuli hiyo. Kuna madimbwi kwenye sakafu. Chini, kuna marundo ya uchafu na takataka.]

## Uhamiaji




Wanafunzi ambao wanalazimika kuhama kwa sababu ya majanga na migogoro katika nchi zao mara nyingi huishia katika kambi za wakimbizi katika nchi nyengine ambapo uwezekano wa kupata elimu unakuwa mdogo. Wanafunzi ambao ni wakimbizi wa ndani ya nchi zao, mara nyingi wana fursa ndogo ya kupata elimu rasmi. Ingawa kwa Zanzibar, wakimbizi wa ndani wanaweza kupata elimu rasmi, lakini kunaweza kuwa na tatizo kubwa la mrundikano wa wanafunzi wengi darasani na hivyo huenda wanafunzi wasipate usaidizi wanaohitaji katika kukabiliana na hali hiyo.

[Maelezo ya picha: Ramani ya muhtasari wa Afrika. Upande wa juu wa ramani kuna mtu aliyekaa kwenye kiti cha magurudumu na nyuma ya kiti hicho kuna njia mbili zinazooonesha kwamba kinatembea. Katikati ya ramani kuna mwanamke aliyeshika mkono wa mtoto na nyuma yake kunaonesha alama za

hatua zikiashiria kutembea. Chini ya ramani kuna mtu anatembea chini na nyayo nyuma yake zinaonesha kutembea. Picha zote ni za kuchorwa.]

## Ulemavu

Wanafunzi wenye ulemavu mara nyingi wanabaguliwa. Hii inaweza kuwa ni sababu ya mitazamo na imani, majengo yasiyofikika kwa urahisi na/au ukosefu wa rasilimali na uwezo wa kusaidia mahitaji mbalimbali ya watoto.




[Maelezo ya picha: Mtoto wa kiume amekaa kwenye kiti cha magurudumu/kitimwendo peke yake akitazama chini. Kuna hatua kadhaa nyuma yake kwenda kwenye mlango wa darasa. Kupitia mlangoni kuna mwalimu anayefundisha.]

## Afya

Afya duni, kutokana na lishe duni na maradhi, huwafanya wanafunzi wengi kutokwenda skuli. Afya duni mara nyingi ni matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo vyengine, kama vile umaskini, majanga na migogoro.

## Jinsia


Ulimwenguni kote bado kuna watoto wa kike wengi zaidi kuliko wa kiume walio nje ya skuli. Mitazamo hasi na baadhi ya tamaduni huathiri watoto wa kike katika kupata elimu. Kwa mfano, ndoa za utotoni na mimba za mapema, hupunguza uwezekano wao wa kwenda au kubaki skuli.




[Maelezo ya picha: Mtoto wa kike ambaye hajavaa sare ya skuli, amebeba mtoto mgongoni. Amesimama nje ya jengo la skuli na kuchungulia ndani. Anaonekana hana furaha. Kuna watoto  wawili wa kike waliovaa sare za skuli wamesimama mbele ya skuli wakimtazama na kuzungumza.]

## Lugha

Lugha ya kufundishia skuli inaweza kuwa ni kikwazo ikiwa ni tofauti na lugha inayozungumzwa nyumbani kwa mtoto ('lugha mama'). Wanafunzi hawa wanaweza kupata tabu katika kujifunza na hatimaye kuacha skuli.





[Maelezo ya picha: Upande wa kushoto kuna Watoto wa kike watatu wamekaa kwa kuelekeana kwa kuzunguka meza na vitabu vilivyofunguliwa vilivyoko mbele yao. Mwanafunzi mmoja wa kike anasema "swali la 2 lilikuwa rahisi", mwengine ana gongo linalomsaidia kutembelea. Msichana wa tatu anamtazama mwalimu aliyesimama karibu yake. Mwalimu anauliza "Je, kuna mtu anahitaji msaada wowote?" Upande wa kulia kuna wanafunzi wawili wa kiume kwenye meza wakiambiana “Umemaliza?” Mwanafunzi wa pili wa kiume amekaa peke yake na kufikiria " je ne comprands pas " (sielewi). Maneno mengine yote yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili.]

## Ukabila, dini na utamaduni

Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuacha skuli ikiwa watakabiliwa na ubaguzi na uonevu kutokana na ukabila au dini zao. Baadhi ya wazazi/walezi wanaweza kuwazuia watoto wao wasiende skuli kwa sababu haizingatii imani za kidini za familia zao au wanahisi kwamba imani zao haziwezi kukubaliwa skuli.

## Umaskini

Katika nchi nyingi duniani umaskini ni kikwazo kikubwa zaidi kinachowafanya wanafunzi kuwa nje ya skuli. Katika maeneo yenye umaskini kwa ujumla kuna skuli chache zenye rasilimali chache na walimu kidogo wenye uhaba wa mafunzo. Masuala haya yanachangia wanafunzi kuwa nje ya skuli. Baadhi ya familia hazina uwezo wa kuwapeleka watoto wao skuli na badala yake wanafunzi wanaweza kulazimika kufanya kazi za kutumikishwa.




[Maelezo ya picha: kuna skuli iliopo ufukweni mwa bahari. nje kuna bango lilioandikwa skuli, kuna wanafunzi wawili waliovaa sare za skuli. Mwanafunzi wa kiume anaonekana akiingia katika eneo la skuli akiwa amevaa mkoba mgongoni kwa mbali upande wa madarasa ya kushoto mtoto wa kike alievaa mkoba anaonekana kuelekea darasani. Ufukweni mwa bahari kuna kijana alievaa bukta anaonekana kunyoosha mkono ili apokee pesa kutoka kwa mwanamke alievaa shungi. Kati kati yao kuna meza iliopangwa samaki. Pembeni kuna mwanamke aliekaa chini akionekana anasafisha samaki, pembeni mwake kuna samaki wengi].

Ulimwenguni kote, ingawa sera zinasema kwamba elimu ni bure, lakini kuna gharama zisizioonekana moja kwa moja, kama vile sare na vitabu.

## 2. Kwa nini wanafunzi wako nje ya skuli Zanzibar?

Kuna sababu nyingi tofauti kwa nini wanafunzi hawaendi skuli Zanzibar. Utafiti kuhusu elimu jumuishi Zanzibar *au* vipengele vya OPD na IETT vya programu ya TOFI vimebaini sababu tofauti zinazoelezea kwa nini wanafunzi hawaendi skuli. Sababu hizo ni pamoja na:

- ukame
- ndoa ya mapema
- mtazamo dhidi ya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, jinsia, ukabila;
- ugonjwa, ulemavu na ukosefu wa huduma za marekebisho
- uraibu wa dawa za kulevya
- kuishi mbali na skuli
- kuonewa
- mazingira ya kusoma yasio salama au kushindwa kusafiri kwa usalama kwenda skuli
- afya dhaifu
- kutoka katika jamii inayobaguliwa ambayo hubaguliwa hata kwenye mfumo wa elimu na afya
- kuwa masikini
- ajira za utotoni; na
- kuwa yatima sisistiza kwamba wanafunzi walio nje ya skuli:
- hawajawahi kwenda skuli, au
- wameacha kabla ya kumaliza, au
- wakati mwengine wanakwenda skuli na wakati mwengine hawaendi

### a) Visa mafunzo vya wanafunzi walio nje ya skuli

Soma visa mafunzo vinavyoelezea wanafunzi tofauti walio nje ya skuli Zanzibar. Fikiria kuhusu:

- Kwa nini mwanafunzi yuko nje ya skuli?
- Kuna vikwazo gani vya kielimu kwa mtoto huyo?
- Jee vikwazo hivi vinaweza kutatuliwa vipi? Je, ni masuluhisho gani yanayowezekana?

**Salma** hutumia kitimwendo. Anataka kwenda skuli ya karibu na marafiki zake wa nyumbani. Skuli hiyo haina njia za kupita kitimwendo, hivyo binamu yake ambaye hakuwa na kazi alifatana naye hadi skuli ili kumsaidia kumpandisha ngazi hadi kwenye mlango. Binamu yake sasa ana kazi na hawezi tena kufuatana naye. Skuli inasema Salmo hawezi kuja skuli bila msaidizi. Salmo amebaki nyumbani tangu wakati huo.

**Daudi** ana tatizo kubwa la kitabia. Alipokwenda skuli, aliweza kutulia darasani kwa dakika 15 tu. Karibu kila siku huwa anafanya utundu darasani. Hali ilimtia matatani zaidi na mara nyingi walimu wake walimtoa darasani. Hatimaye aliacha kuja skuli. Sasa haendi skuli tena lakini mara nyingi hukaa katika mji wa karibu na watoto wakubwa zaidi kuliko yeye na amekuwa akiingia matatani na wauza maduka na polisi.

**Tawfiiq** amepata ulemavu wa uoni na matatizo ya kujifunza. Wazazi wake wanaona aibu kwa kuwa na mtoto huyo. Wanaishi mbali na skuli hivyo anasaidiana na familia yake kuuza mbogamboga katika soko la karibu na hajawahi kwenda skuli.

**Halima** ana miaka 12. Anaishi na familia yake ya watoto tisa katika vyumba viwili vidogo. Hakuna hata mmoja katika familia hiyo ambae amekwenda skuli. Mama yake hutembea kilomita 6 kila siku kutafuta mabaki ya chakula katika mji wa karibu ili kuongeza chakula cha familia. Wakati fulani Halima hutumwa kuuza njugu zilizokaangwa kwenye kituo cha malori kilichopo karibu.

**Amina** hajui kusoma wala kuandika na aliacha skuli akiwa na umri wa miaka 9. Alilazimishwa kuolewa alipokuwa na miaka 14. Familia ya Amina ni maskini sana na walimuozesha mume ili kuiletea familia pesa na ulinzi. Amina bado anaishi na familia yake.

# 3. Sera ni nini?


Vikwazo vingi vinawasababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli. Lakini Zanzibar, kama ilivyo katika nchi nyingi, elimu ni haki kwa wanafunzi wote. Ni muhimu kufahamu ni sera zipi zimewekwa Zanzibar zinazolinda haki ya watoto wote ya kupata elimu. Tunaweza kutumia sera hizi kutetea haki za watoto ambao wako nje ya skuli. Lakini ili kuzitumia ipasavyo tunahitaji KUANGALIA wanachosema na KUFIKIRI jinsi tunavyoweza kuzitumia vizuri.

## Sera zinaweza kuwa za aina nyingi

- Sera inaweza kuwa seti ya **kanuni za kufanyia kazi** ili kuongoza kikundi cha watu au jumuiya (kwa mfano, sera ya skuli kuhusu utoro wa walimu au kanuni za kikundi cha vijana).
- Sera inaweza kuwa na maana ya seti ya **mikakati** inayoelezea kitu ambacho serikali inapanga kufanya mabadiliko (kwa mfano, sera ya elimu mjumuisho au sera ya kuimarisha sifa za walimu).
- Sera inaweza kuwa **sheria** inayoongoza mfumo wa kisheria wa nchi (Kwa mfano, sheria inayolinda watu dhidi ya ubaguzi).
- Sera zinaweza kuwa na **malengo ya muda mfupi, wa kati au mrefu.**
- Sera tunazosoma **huwa na historia zake** - ni nani aliyehusika katika kuandaa sera hii? Je, kulikuwa na masuala ambayo watu walitofautiana nayo na watu walikubaliana vipi juu ya sera?
- Kwa hivyo, tunapoangalia sera **tunahitaji KUANGALIA na KUFIKIRI** kwa makini.

Sera zinaweza kufanya kazi katika **ngazi tofauti** (kwa mfano, zinaweza kuongoza utendaji katika skuli au zinaweza kufanya kazi katika ngazi ya kimataifa ili kuongoza nchi mbalimbali, kama vile Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu)

## Ni nini sera?




[Maelezo ya picha: Slaidi inaonesha picha tatu zilizowekwa moja pembeni ya nyengine. Picha ya kwanza iliyopo kushoto inaonesha Katiba ya Zanzibar. Ina rangi ya kijani iliokoza kwa maandishi ya dhahabu. Juu ya jalada kuna nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katikati imeandikwa Katiba ya Zanzibar ya 1984 na chini kabisa imeandikwa toleo la 2010. Pembeni ya picha hii kuna picha nyengine ya Sera ya elimu. Sera hio juu ina nembo ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya nembo hio kuna maneno yalioandikwa kwa Kiingereza yanayosema Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, chini yake imeandikwa Wizara ya elimu na mafunzo ya amali. Chini ya maneno hayo kuna picha zilizokusanywa pamoja zinazoonesha majengo ya skuli na wanafunzi wakiwa madarasani. Chini ya picha hio kuna 2006 kuashiria mwaka iliopitishwa sera hio. Pembeni ya picha hio kuna picha nyengine yenye rangi nyeupe juu ikiwa na rangi nyeusi na chini kabisa ina rangi ya buluu na ya kijani. Juu kuna nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na maneno hayo yameandikwa kwa Kiingereza chini ya nembo hio. Chini yake kuna maneno mengine yakiingereza yanayosema Ofisi ya makamo wa pili wa Rais, na chini yake kuna maneno yanayosema sera ya watu wenye ulemavu Zanzibar. Na chini yake kuna 2018 kuashiria mwaka iliopitishwa Sera hio.]

# 4. Mikakati na suluhisho la kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli

Wakati mwingine hata kama tunajua ni kwa nini watoto hawendi skuli na aina ya vikwazo wanavyokabiliana navyo, hatujui watoto walio nje ya skuli katika jumuiya zetu wako wapi na vikwazo mahususi wanavyokabiliana navyo. Kwa hivyo, ni muhimu kutafuta njia za kuwapata na kuwatambua watoto walio nje ya skuli katika jamii. Kisha tunaweza kufanya kazi kutafuta suluhu ya kuwarejesha skuli. Tunaweza kutumia mzunguko wa CHUNGUZA, FIKIRIA, TENDA kulifanyia kazi suala hili.

Hapa kuna baadhi ya zana na ujuzi mzuri tunaoweza kuutumia kuangalia na kufikiria ni wapi wanafunzi walio nje ya skuli wanaweza kuwepo, kwa nini hawako skuli na ni suluhisho gani tunaweza kutumia.

**Mahojiano na Vikundi Lengwa:** Njia nzuri ya kukusanyia taarifa kutoka kwa watu katika jamii kuhusu mahali walipo watoto walio nje ya skuli na aina gani ya vikwazo wanavyokabiliana navyo, ni kutengeneza mahojiano au vikundi lengwa. Kumbuka kwamba ni muhimu kutumia maswali ya wazi katika mahojiano na makundi lengwa watu hujisikia huru kuwa wawazi kuzungumzia kuhusu wanachokijua na kufikiria.

**Stadi za kusikiliza:** Stadi nzuri za kusikiliza ni muhimu sana katika kukusanya taarifa kuhusu kile ambacho watu wanafahamu kuhusiana na watoto ambao wako nje ya skuli, na wapi tunaweza kuwapata. Stadi nzuri za kusikiliza zitatusaidia pia kuelewa vizuri vikwazo ambavyo watoto na familia wanaweza kukumbana navyo.



Washiriki wakifanya mazoezi ya stadi za kusikiliza wakati wa mafunzo huko

[Maelezo ya picha. Picha inaonesha wanawake wawili wamekaa kwa kuelekeana. Mmoja anasikiliza huku mwengine akizungumza.]

**Uchunguzi (kutazama):** Uchunguzi ni sehemu muhimu ya hatua ya 'CHUNGUZA' ya mzunguko wa 'CHUNGUZA-FIKIRI-TENDA'. Kunaweza kuwa na mahali katika jamii ambapo tunaweza kuona wanafunzi walioko nje ya skuli na kuchunguza kwa nini hawaendi skuli (k.m. sokoni wakati ni siku ya skuli - kuangalia wanafunzi ambao hawajaenda skuli wakiuza mbogamboga).

**Kuchora ramani:** Kuchora ramani kunaweza pia kusaidia kutambua mahali ambapo watoto walio nje ya skuli wanapatikana katika jamii na vikwazo wanavyokumbana navyo. Kuchora ramani kunaweza kusaidia kujenga taswira ya ukubwa wa tatizo. Hii inaweza kusaidia katika kupanga suluhu na kufikiria ni nani katika jamii anaweza kusaidia kuwarudisha watoto skuli.




Mfano wa ramani ya skuli iliyotengenezwa Pemba


[Maelezo ya picha: ramani inaonesha mitaa katika mpangilio huo wa mitaa yapo maumbo mbalimbali ya mraba yenye kuonesha nyumba, maduka na skuli. Kuna alama zenye kuonesha vikwazo vya ujumuishi.]

# 5. Uhamaji katika elimu ni nini?

Uhamaji katika elimu ni pale wanafunzi wanapofika au wanaporudi kutoka skuli. Ni wakati wanakwenda skuli kwa mara ya kwanza, au kuhama kutoka darasa moja au skuli moja kwenda nyengine.


Kipindi hiki huathiri wanafunzi kwa njia tofauti. Uzoefu mwingi wa uhamaji kwa wanafunzi ni chanya lakini wakati mwengine huwa hasi na wanafunzi wanaweza kuendelea kukabiliana na matatizo.

Wanafunzi wengine huacha skuli wakati au punde tu baada ya kipindi hiki cha mpito, hususan ikiwa wana mahitaji maalumu ambayo hayajashughulikiwa wakati wa mchakato wa kipindi cha mpito.




[Maelezo ya picha: Kijana wa kiume aliyevaa sare ya skuli, ana mkoba wa skuli na anapanda hatua kadhaa. Maneno ‘Skuli ya Sekondari’ yameandikwa juu ya ngazi. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Watoto hao ni pamoja na kijana wa kiume aliyevaa shuka kiunoni akimtazama mwenzake juu, kijana mmoja wa kike amembeba mtoto mgongoni akionekana hana furaha na kijana wa kiume aliyevaa miwani ya myeusi, akiwa ameshika fimbo na kutazama upande mwengine. Maneno ‘skuli ya msingi’ yameandikwa chini ya ngazi.]

Kipindi cha uhamaji katika elimu kinahusisha watoto kuhama kutoka nyumbani hadi skuli, au kuhamia skuli (kwa mfano, kutoka skuli ya msingi darasa la 5 kwenda darasa la 6) au kutoka skuli moja hadi nyengine (kwa mfano, kuondoka skuli ya msingi na kujiunga na skuli ya sekondari). Mabadiliko haya yanatoa fursa na changamoto za kujifunza na maendeleo ya watoto. Kudhibiti mabadiliko kwa pamoja huwasaidia watoto wote kunufaika kutokana na mabadiliko wanayopata.




[Maelezo ya picha: Katika kona ya juu kushoto, kuna jengo lililoandikwa 'Skuli ya msingi'. Mtoto mdogo wa kike mwenye fimbo anatembea kwenye njia kuelekea skuli ya msingi. Kulia hapa kuna jengo lililoandikwa 'skuli ya Sekandari. Mtoto huyo huyo akionekana mkubwa sasa anatembea kwenye njia kutoka skuli ya msingi kuelekea skuli ya sekondari . Chini kuna jengo lililoandikwa 'Chuo'. Kijana wa kike mwenye fimbo nyeupe anatembea kwenye njia kutoka skuli ya sekondari kuelekea chuo kikuu.]

Zanzibar skuli hufungwa mara kwa mara kutokana na mafuriko, ukame, na baadhi ya wakati uhaba wa chakula. Hii ndiyo inasababisha wanafunzi wengi kulazimika kurudi tena skuli baada ya kukosa kuhudhuria kwa muda mrefu. Ingawa ni vyema kuona kwamba skuli zinafunguliwa tena, kuna changamoto kwa wanafunzi, familia zao, skuli na walimu. Wanafunzi wengine hupelekwa katika madarasa mengine moja kwa moja bila maandalizi yanayoweza kusaidia kukabiliana na ngazi nyengine ya darasa. Kuongezeka kwa uandikishaji kunaweza pia kusababisha msongamano mkubwa madarasani na wengine wanaweza kupata shida katika  kushiriki na kufaulu katika mazingira kama haya.

## a) Walichosema wanafunzi kuhusu kipindi cha uhamaji

Haya ni baadhi ya mambo ambayo wanafunzi wamesema kuhusu uzoefu wao wa uhamaji katika elimu.

Sijui pa kwenda wala kujua njia ya kwendea skuli yangu mpya

Nina wasiwasi sitapata marafiki wapya au kushiriki kikamilifu katika matukio ya skuli.

Wazazi wangu hawashirikishwi sana katika elimu yangu. Niko darasa la juu, lakini bado ninataka nizungumze na walimu wangu

Sikuona ndani ya skuli yangu mpya hadi siku ya kwanza ya muhula. Niliogopa.

Nimechanganyikiwa na ratiba mpya. Ninapaswa kwenda wapi na lini? Naambiwa kwa kuchelewa.

Kila mtu anadhani mimi ni 'mkubwa' naweza kustahimili katika skuli yangu mpya. Bado ninaogopa na kuchanganyikiwa!



Skuli iko katika kitongoji tofauti - hiyo inatisha.

Ninapata shida kwa kuwa mkorofi kwa mwalimu wangu mpya kwa sababu sielewi anataka nifanye nini.

Ni vigumu sana kuhitimu hadi ngazi nyengine. Mtihani haujarekebishwa kulingana na mahitaji yangu.

Walimu katika skuli yangu ya zamani walipanga jinsi ya kunisaidia katika masomo fulani. Skuli yangu mpya haijui kuhusu hili. Mipango yote ya usaidizi lazima ianzishwe tena. Natamani mwalimu wangu wa zamani bado angehusika.

Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu siku nzima.

Nataka kwenda chuo cha ufundi. Sijui ni vyuo gani vinajumuisha wanafunzi wenye ulemavu. Hakuna mtu katika skuli yangu anajua pia.

Walimu hufanya mambo tofauti katika skuli hii. Wana njia tofauti za kufundishia. Siwezi kuzoea matarajio yao.

## b) Athari za kipindi cha mpito katika elimu kwa wanafunzi

Kuna aina mbalimbali za athari chanya na hasi zinazotokana na mpito katika elimu kwa wanafunzi. Baadhi ya athari hizi zimeorodheshwa hapa chini:

**Athari Chanya zinazotokana na kipindi cha mpito**

Wanafunzi kutoka elimu ya msingi Kwenda sekondari, inaelezwa kuwa

- Walikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi ya kuhimili kazi, lakini walifurahia kuwa na masomo zaidi ya kusoma, hasa yale yanayohusisha kufanya na kutengeneza, kama vile sayansi, sanaa, pamoja na usanifu na teknolojia.
- Walihuzunika kumuacha mwalimu wao wa skuli ya msingi lakini walitazamia kufundishwa na walimu maalum wa masomo mbalimbali
- Walikuwa na wasiwasi kuhusu kuwapoteza marafiki wao wa zamani kutoka skuli ya msingi lakini walifurahia kujenga uhusiano mpya

Vijana wanaweza kuwa katika hatari ya msongo wa mawazo fulani, lakini pia wanaweza kutamani mabadiliko, uhuru zaidi, na uzoefu mpya.

**Madhara hasi ya kipindi cha mpito/mabadiliko**

Baadhi ya wanafunzi, hasa wenye ulemavu, wanaweza kukumbwa na vitendo vya unyanyasaji.

Mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu yanahitaji mipango ya kina;
Bila mipango hii, wanaweza kukosa msaada na uelewa wanaohitaji.

Wakati mwingine mwalimu mpya hajui mipango ya kuwasaidia wanafunzi kama mipango ya skuli aliyotoka.

Baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu hukumbwa na changamoto ya ufikiaji au kuzunguka skuli mpya.

- Watoto wakike wanaweza kukumbwa na msukumo wa aina mbalimbali wanapobadilishwa kutoka skuli ya msingi kwenda sekondari, hali ambayo inaweza kusababisha kuacha skuli. Mfano wa changamoto hizo ni kuongezeka kwa kazi za nyumbani au shinikizo la kijamii la kuolewa.


- Wasichana wanapoanza hedhi, hali hii inaweza kusababisha kutohudhuria masomo kama inavyotakiwa.
- Baadhi ya Watoto wakike wanapoendelea na masomo yao ya sekondari huripotiwa kujihisi kutoweza kufaulu na huachwa nyuma kitaaluma.
- Maendeleo ya kitaaluma yanaweza kupungua katika wiki za mwanzo za mwanafunzi anapojiunga na skuli mpya. Ikiwa mwanafunzi ataachwa nyuma, anaweza kujihisi kukosa motisha au kuvunjika moyo.
- Wanafunzi wanaowasili katikati ya mwaka au muhula wa masomo (kwa mfano, waliopata uhamisho wa makazi, wakimbizi wa ndani au wakimbizi kutoka nje) hawapati msaada sawa na wanafunzi wanaoanza skuli mwanzoni mwa mwaka wa masomo.
- Iwapo wazazi/walezi hawahusishwi katika maisha ya skuli mpya, hali hii inaweza kuongeza tafauti za kijamii.

# 6. Kipindi cha uhamaji jumuishi huanzia nyumbani

**Wazazi na familia** daima ni sehemu muhimu ya elimu kwa watoto. Familia, nyumbani na jamii hubaki kuwa sehemu muhimu kwa mtoto anapohama sehemu moja ya kielimu kwenda nyengine.


Kwenda skuli haimaanishi ni mwisho wa kujifunza nyumbani. Ili kuhakikisha kwamba uhamaji unakuwa mzuri na jumuishi ni muhimu kuwahusisha wazazi na walezi.

Wazazi na familia mara nyingi huwa watetezi wa kwanza wa elimu ya watoto wao. Wanaweza kuwachagulia skuli, wakitetea skuli kutambua na kukidhi mahitaji ya mtoto wao, wakihakikisha mtoto wao ana nyenzo zote anazohitaji ili kujumuishwa kikamilifu, na kumuandaa mtoto wao kwa mabadiliko. Pia ni watu wanaojua zaidi mahitaji ya usaidizi wa mtoto wao. Haya yote ni majukumu muhimu ambayo wazazi na familia hutekeleza wakati wa kipindi cha mpito wa kielimu.




[Maelezo ya picha: Kuna watu wamekaa juu ya viti, nje ya jengo la skuli. Wanajumuisha watu wanaotambulika katika jamii, kamati ya elimu mjumuisho ya skuli na mwalimu mkuu. Mwanamke mmoja amesimama katikati akihutubia watu. Pembeni yake kuna mwanamme aliyemshika mkono mtoto wa kiume aliyevaa sare za skuli akiwa ameshika fimbo ndefu. Watu waliokaa kwenye viti wote wanamsikiliza kwa makini mwanamke huyo akizungumza.]

**Familia, nyumbani na jamii zinabaki kuwa sehemu muhimu kwa mwanafunzi kadri anavyo kwenda katika ngazi tofauti za kielimu**



[Maelezo ya picha: Picha inaonesha kikundi cha wanafamilia katikati majengo manne katika kila kona, yenye njia na mishale inayounganisha majengo na familia. Familia hiyo inajumuisha mtoto mdogo na mkubwa wa kike na kijana wa kiume mkubwa, mzee mwenye fimbo, mwanamke mtu mzima na mwanamme mtu mzima. Maneno ‘familia na nyumbani’ yako chini ya kikundi cha familia. Kwenye kona ya juu kushoto, kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya maandalizi’.

Watoto wawili wa kike; mdogo na mkubwa walioshikana mikono wanatembea kwenye njia ya kuelekea ' skuli ya maandalizi '. Kuna mshale uliopinda kutoka skuli ya maandalizi hadi kona ya juu kulia ambapo kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya msingi’. Mtoto huyo huyo wa kike anaonekana akitembea kwenye njia kutoka katika familia kuelekea skuli ya msingi. Kuna mshale uliopinda kutoka skuli ya msingi hadi kona ya chini kulia ambapo kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya sekondari’.

Msichana yuleyule akionekana mkubwa sasa anatembea kwenye njia kutoka katika familia yake kuelekea skuli ya sekondari. Mwisho, kuna mshale uliopinda kwenye kona ya chini kushoto ambapo kuna jengo lililoandikwa ‘chuo kikuu’. Mwanamke mmoja anatembea kwenye njia kutoka kwa familia yake kuelekea chuo kikuu.]

## a) Kabla ya kufika skuli

Kuna mambo katika maisha ya nyumbani ya watoto ambayo huathiri mahudhurio yao au ushiriki wao katika elimu wanapoondoka kutoka nyumbani kwenda skuli kila siku.

Mambo matatu muhimu ni:

- kulala,
- kifungua kinywa
- kazi za nyumbani.

### Kulala

Kulala kwa muda wa kutosha ni muhimu kwa watoto wote. Uchovu huathiri kujifunza na ustawi. Inaweza kusababisha kutokuwa makini na kutokuwa na kumbukumbu darasani. Inaweza pia kuathiri vibaya hali za watoto za kihisia na kiwiliwili.



[Maelezo ya picha: Kuna meza mbili na watoto watatu wamekaa katika kila meza. Upande wa kushoto nyuma kuna Watoto wa kike watatu wamekaa pamoja. Vitabu vyao viko wazi na wanazungumza; mmoja ana gongo linalomsaidia kutembea. Kwa nyuma ukutani kuna mabango yenye maandishi. Kwenye meza ya mbele ya kulia kuna watoto wa kiume watatu. Mtoto wa kiume upande wa kushoto ana miwani myeusi na fimbo nyeupe. Mtoto wa kiume aliye upande wa kulia amelala na kichwa chake kikiwa juu ya meza.]

## Kifungua kinywa/chai

Kama vile kukosa usingizi, njaa huathiri umakini na afya ya watoto. Baadhi ya skuli hufanya kazi na jumuiya za ndani ili kuunda klabu zinazoshughulikia masuala ya kupata chai au programu za lishe katika skuli. Wakati mwengine wanapokea msaada kutoka kwa wanajamii au wafanyabiashara wa karibu.




[Maelezo ya picha: Upande wa kushoto kuna Watoto wa kike waliovaa sare za skuli wamekaa ndani ya darasa kwenye meza wakila chakula. Kupitia mlango ulio wazi upande wa kulia kuna watoto wa kiume wamekaa nje kwenye viti wakila chakula. Mtoto mmoja wa kiume yuko kwenye kiti mwendo na mwanamme mmoja anampa chakula. Upande wa kushoto kabisa kuna sufuria mbili kubwa juu ya jiko na zinatoa mvuke. Kuna mwanamke nyuma ya sufuria akihudumia chakula. Watoto zaidi wanajikusanyia sahani za chakula. Kuna mwanamke anatembea amebeba sahani. Ishara inasema 'Skuli' mbele kushoto ya picha. Eneo lina shughuli nyingi].

## Kazi za nyumbani

Kusaidia ndani na nje ya nyumba kunaweza kuwa sehemu muhimu ya kujifunza ujuzi mpya na kuwajibika. Inaweza pia kuathiri vibaya elimu kwa kuwafanya watoto kuchoka, kuwa wachafu au kuchelewa skuli.



[Maelezo ya picha: Kijana mdogo wa kike anasafisha sakafu ya chumba na ndoo iliyo karibu naye. Kuna sofa nyuma yake na picha mbili ukutani, moja ikionesha watu wanne (watu wazima wawili na watoto wawili) na moja ikionesha watoto wawili. Kijana wa kiume anapita karibu na msichana akisafisha sakafu. Amevaa sare za skuli na ana mkoba wa mgongoni. Kuna mtoto wa kike anamtazama. Anaonekana hana furaha.]

# 7. Mikakati ya kusaidia uhamaji jumuishi

Skuli pia zina jukumu la kusaidia kipindi cha kuhama kutoka sehemu moja Kwenda nyengine kuwa jumuishi. Kuna mikakati tofauti ambayo skuli inaweza kuweka ili kusaidia kipindi hiki kuwa jumuishi. Mikakati hiyo ni pamoja na vitu kama vile:

- Kuweka utaratibu wa wanafunzi kusaidiana hasa wanapokuja wanafunzi wapya. Wahimize wanafunzi kusaidiana na wazawadie kwa kutoa usaidizi huo.
- Kupanga wanafunzi waweze kutembelea darasa la wenzao au skuli na kufahamu mazingira, watu na taratibu kabla ya kuhama.
- Kuandaa sera ya kupinga unyanyasaji na kuhakikisha kunakuwa na watu wazima wanaoshughulikia chai na chakula cha mchana skuli ili waambiwe kwamba kuna wanafunzi wapya watakuja.

Pia kuna mikakati maalum inayohusisha kushirikiana na wazazi/walezi na familia za mwanafunzi, kwa mfano:

Ziara za nyumbani zinazofanywa na walimu au wajumbe wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli. Hii inaweza kumsaidia mwalimu kumfahamu mwanafunzi na kusaidia kushughulikia matatizo ya wazazi/mlezi:




[Maelezo ya picha: Kuna watoto watatu wanacheza nje. Vijana wawili wa kiume na mmoja wa kike. Kijana mkubwa wa kiume upande wa kushoto anaonekana kama anaashiria kupiga mpira . Kuna mpira mbele yake. Mvulana aliyevaa fulana ya njano yuko upande wa kulia na anatembea kuelekea kwenye mpira; ana fimbo ndefu. Msichana amekaa upande wa kushoto kabisa, akipiga makofi na kumtia moyo. Nyuma yao kuna mwanamme na mwanamke wanaotazama na kutabasamu.]

**Kutoa taarifa, usaidizi na nyenzo za uhamasishaji** kuhusu skuli ili kushughulikia matatizo ya familia na kuwahimiza kuwa wao ni sehemu muhimu/hai ya mchakato wa mpito.




[Maelezo ya picha: Kuna watu watatu wamesimama wakizungumza nje. Mwanamke mmoja anawapa wenzake vikaratasi vya rangi ya njano. Mwanamme aliye karibu anabandika bango la manjano linaloitwa 'skuli jumuishi' nje ya jengo. Huku nyuma mwanamme mwengine anawapa vipeperushi watu wawili ambao wamekaa na kuzungumza. Huku nyuma kuna mbuzi na kuna nyumba za kijijini, mtu mzima na kijana wa kiume wanalima bustani].

**Kufanya kipindi elekezi** (kualika familia kutembelea skuli) labda kama sehemu ya siku ya kujiandikisha skuli. Hii inaweza kusaidia kuwatambulisha wazazi na walezi skuli na kushughulikia matatizo na kuwahimiza kuwa sehemu hai ya mchakato wa mpito.




[Maelezo ya picha: Watu wengi wamekusanyika nje, mbele ya jengo la skuli. Upande wa kushoto kuna mwanamke aliyekaa kwenye dawati huku pembeni yake kukiwa na alama ya ‘uandikishaji’. Kuna wanawake wawili na watoto wawili wamesimama mbele ya dawati. Kwa nyuma, mbele ya skuli, kuna wavulana wawili wamebeba meza ndani ya darasa. Upande wa kushoto nyuma ya dawati, wavulana watatu, akiwemo mmoja mwenye gongo la kumsaidia kutembea wanacheza mpira wa miguu. Upande wa kulia, baadhi ya watu wamekusanyika kwenye viti chini ya hema na wanamsikiliza mwanamke akizungumza.]

## a) Kanuni kuu za mabadiliko

- Wanafunzi wote wanastahiki na wana haki ya kufurahia uhamaji mzuri kutoka ngazi moja ya kieleimu kuelekea nyengine.
- Mahusiano mazuri ni muhimu: mabadiliko yanayofaa yanategemea kuaminiana na kuheshimiana kati ya mtoto, mzazi na wataalamu wote wanaohusika.
- Kila mwanafunzi ni mtu binafsi: usaidizi wa uhamaji unapaswa kubadilika kulingana na mahitaji ya mwanafunzi.
- Usaidizi ulioratibiwa na mawasiliano mazuri kati ya walimu na jumuiya ni muhimu
- Mazingira ya skuli yanasaidia mawasiliano ya wazi, ya kuaminiana na ya uaminifu na yanahimiza ushirikiano
- Muda na rasilimali za kutosha zimetengwa ili kuhakikisha uandikishaji, tathmini ya awali na usaidizi wa mafunzo unafaa.
- Wanafunzi wanasikilizwa, hata wawe wadogo, ili mahitaji yao yaeleweke na maoni yao yazingatiwe
- Familia zinahusika katika kupanga: wazazi/walezi ni chanzo muhimu cha taarifa na usaidizi kwa skuli.

# 8. Jukumu la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu katika kutambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi

Uhamaji jumuishi huanzia nyumbani na katika jamii na kuendelea na safari ya kwenda skuli, kufika skuli na darasani. Kusaidia mpito jumuishi ni wajibu wa wazazi na walezi pamoja na wafanyakazi wa skuli na walimu.

Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu ina jukumu muhimu la kutekeleza katika kutambua wanafunzi walio nje ya skuli na kuwezesha uhamaji ulio jumuishi. Jukumu hili linaweza kuwa na namna tofauti. Baadhi ya mambo muhimu wanayoweza kufanya ni:

A. **Kutumia sera kushawishi ufanyaji maamuzi kwa ajili ya mabadiliko.**
B. **Kutafuta na kukusanya taarifa ili kuwa na ushahidi wa kuleta mabadiliko.**
C. **Kuwezesha ushirikiano ili kujenga umoja imara na mitandao kwa ajili ya mabadiliko.**
D. **Kuongeza ufahamu kuhusu mabadiliko gani yanahitajika kwa elimu mjumuisho.**
E. **Kufuatilia na kusaidia michakato ya mabadiliko ya elimu mjumuisho.**

## A. Kutumia sera kushawishi ufanyaji maamuzi kwa ajili ya mabadiliko




[Maelezo ya picha: Kuna watu watano wamekaa katika chumba. Kuna kalenda kwenye ukuta. Upande wa kulia kuna mwanamme aliyevalia nadhifu amekaa nyuma ya dawati na karatasi kadhaa juu yake. Maneno 'Afisa Elimu wa Wilaya' yameandikwa kwenye dawati.

Anasikiliza. Wanaotazamana naye ni watu wanne wamekaa kwenye viti. Mwanamme aliye karibu naye ni mwanamke aliyevalia vizuri na fimbo ndefu nyeupe. Anaashiria na kumweleza mwanamme jambo fulani. Ameshika karatasi rasmi za serikali zenye nembo. Pembeni yake kuna mvulana aliyeshika fimbo nyeupe na mwanamme pamoja na mwanamke. Wanatabasamu.]

## B. Kutafuta na kukusanya taarifa ili kuwa na ushahidi wa kufanya mabadiliko




[Maelezo ya picha: Mwanamme mwenye mguu mmoja, amevaa suti na kutumia gongo linalomsaidia kutembea. Amesimama nje kidogo ya mlango wa nyumba. Mlango uko wazi. Mwanamke amesimama kwenye mlango ulio wazi akizungumza na mwanamme. Amevaa nguo za msingi. Anaashiria na nyusi zake zimeinuliwa - kama vile anaelezea jambo fulani. Nyuma yake, kupitia mlango ulio wazi msichana mdogo anasafisha sakafu.]

## C. Kuwezesha ushirikiano ili kujenga umoja imara na mitandao kwa ajili ya mabadiliko



[Maelezo ya picha: Kuna watu 9 wamekaa katika nusu-duara kwenye viti kwenye chumba chenye madirisha matatu nyuma. Kupitia madirisha unaweza kuona baadhi ya majengo yanayofanana na majengo ya skuli. Katika kikundi hicho kuna mwanamme mwenye kiti mwendo, mwanamme mzee mwenye fimbo na msichana aliyevaa sare za skuli na mwenye mguu mmoja na gongo la kumsaidia kutembea, pamoja na wanawake wengine watatu na mwanamme na mvulana mdogo waliovalia miwani nyeusi wakiwwameshika fimbo ndefu. Kikundi kinamsikiliza mwanamke mmoja akiongea na wana sura nzito na zenye wasiwasi.]

## D. Kuongeza ufahamu kuhusu mabadiliko gani yanahitajika kwa elimu mjumuisho



[Maelezo ya picha: Kundi la watu wanane wamekusanyika pamoja nje. Watu wengine wamekaa na wengine wamesimama. Mwanamke mmoja amekaa ana fimbo inayotumiwa na watu wasioona. Mwanamke mwengine amesimama anafanya ishara kwa mikono yake na kuwasiliana na mwanamme. Watu wote wanatazama na kumsikiliza mwanamke aliyevalia nadhifu ambaye amesimama, akitabasamu na kuzungumza kwa kutumia kipaza sauti.

Amemzungushia mkono wake msichana mdogo alievaa mavazi ya rangi ya zambarau na ana mkoba. Msichana anamtazama na kutabasamu. Mwanamme aliyevaa suti ambae ana mguu mmoja amekaa kwenye kiti karibu na mwanamke mwenye kipaza sauti. Gongo limewekwa chini. Kwa nyuma kuna maduka, msikiti, watu wanatembea na watu wamekaa chini wakionesha marundo ya mazao.]

## E. Kufuatilia na kusaidia michakato ya mabadiliko ya elimu mjumuisho




[Maelezo ya picha: Kuna watu wengi, wanaume, wanawake na watoto wanaofanya kazi pamoja mbele ya jengo la skuli. Mwanamme anasukuma toroli lenye mawe makubwa ndani yake. Baadhi ya watu wanaweka mawe ili kutengeneza kingo za njia zinazoelekea shuleni.

Mvulana aliyekaa kwenye kitimwendo anaelekeza mahali pa kuweka mawe. Huku nyuma wanawake wawili waliovalia nadhifu wanazungumza. Mvulana mwenye fimbo nyeupe anatembea karibu na mwanamke ambaye amebeba sanduku la chupa za maji.]